

## **MKATABA WA KUPANGISHA PANGO (FREMU YA BIASHARA)**

Mkataba huu unafanyika leo tarehe 20 Mwezi 11 mwaka 2025

### **KATI YA**

JOHN SAMWELI MUSA anayeishi Dar es Salaam, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MPANGISHAJI"**) Kwa upande mmoja, ambapo itajumuisha familia na warithi wake wote;

**NA**

RAWASI TRANSPORTERS LIMITED mwenye sanduku la barua s **Dar Es Salaam,** Tanzania, ambaye katika mkataba huu atatambulika kama **("MPANGAJI")** Kwa upande wa pili;

### **UTANGULIZI WA MKATABA;**

a) **KWAMBA**, Mpangishaji anayo nia thabiti na yuko tayari kupangisha FREMU yake iliyopo

mtaa wa SINZA A Wilaya ya UBUNGO jijini DAR ES SALAAM

b) Muda wa Mkataba utakuwa ni wa miezi kumi na mbili ambapo pande zote mbili zimekubaliana. Mkataba mwingine unaweza kufanyika baada ya huu kumalizika.

c) **KWAMBA**, Mpangaji yuko tayari kupangishwa na Mpangishaji wa fremu hii tajwa ili kutumia kama ofisi ya biashara.

d) **KWAMBA**, pande zote mbili ziko tayari kuzingatia masharti ya Mkataba huu na kuyatekeleza ipasavyo.

### **KWA HIYO MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

1. **KWAMBA**, kodi itakayolipwa na Mpangaji kwa Mpangishaji katika Mkataba huu wa upangishaji ni Shilingi za Kitanzania 2,400,000 ikiwa ni kodi ya **Miezi kumi na mbili (12)** ambapo kila mwezi ni Shilingi 200,000
2. **KWAMBA**, Mpangaji anamkabidhi pesa hizi taslim Mpangishaji baada ya kutia sahihi katika mkataba huu wa upangishaji.
3. **KWAMBA**, Mpangishaji atamkabidhi rasmi fremu hii ya biashara Mpangaji ikiwa haina migogoro ya aina yeyote na anamuahidi Mpangaji kuwa endapo itajitokeza shida ya aina yoyote ile, basi Mpangishaji atasimama na kutetea maslahi ya Mpangaji.
4. **KWAMBA**, Mpangaji anaahidi kutumia fremu hii kwa biashara na kuiweka fremu hii katika mazingira mazuri muda wote wa upangaji wake.
5. **KWAMBA**, Mpangishaji endapo atataka kufanya marekebisho yoyote kwenye fremu yake, atampatia taarifa Mpangaji na Mpangaji pia endapo atataka kufanya maboresho yoyote katika fremu hii atampatia taarifa Mpangishaji kabla ya kufanya chochote.
6. **KWAMBA**, Kama kutakuwa na ukiukaji wowote wa mkataba huu pande zote mbili zitataarifiana **miezi miwili (2)** kabla ya mkataba huu kufikia ukomo ili pande zote mbili ziweze kujipanga na mabadiliko yanayojitokeza.

7. **KWAMBA**, endapo Mpangaji atapoteza haki zake kama Mpangaji kwa namna yeyote ile kutokana na Mpangishaji kutokuwa mmiliki halali wa eneo hili tajwa, Mpangishaji atalazimika kumlipa Mpangaji fidia ya gharama zote alizoingia tangu kuanza kwa mchakato huu wa upangishaji pamoja na pesa zake zote na Mpangaji anaahidi kumchukulia Mpangishaji hatua kali za kisheria dhidi yake.

**UMESAINIWA NA:-**

JOHN SAMWELI MUSA



.....  
**MPANGISHAJI**

**UMESAINIWA NA:**

RAWASI TRANSPORTERS LIMITED  
(BRENDA SIMON MWASIPU)



.....  
**MPANGAJI**

**UMESHUHUDIWA MBELE YA:**

**Jina** YONA LUCIAN HABIYE

**Anuani** BOX 60022 DSM

**Wasifu** WAKILI



